JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI

# TAARIFA KWA UMMA KUHUSU TAASISI NA ASASI ZA KIRAIA ZILIZOPATA KIBALI CHA KUTOA ELIMU YA MPIGA KURA NA UANGALIZI WAKATI WA UCHAGUZI MDOGO WA UBUNGE KATIKA JIMBO LA PERAMIHO, HALMASHAURI YA WILAYA YA SONGEA NA UDIWANI KATIKA KATA YA SHIWINGA, JIMBO LA MBOZI, HALMASHAURI YA WILAYA YA MBOZI

**Dodoma, 30 Januari, 2026**

Kwa mujibu wa kifungu cha 10(1)(h) cha Sheria ya Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 292 kikisomwa pamoja na kanuni ya 22 (4) ya Kanuni za Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi za Mwaka 2024, Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi katika kikao chake cha tarehe 30 Januari, 2026 imetoa kibali cha kutoa elimu ya mpiga kura wakati wa Uchaguzi Mdogo wa Ubunge katika Jimbo la Peramiho na Udiwani katika Kata ya Shiwinga kwa taasisi na asasi za kiraia sita (06).

Aidha, kwa mujibu wa kifungu cha 85(4) cha Sheria ya Uchaguzi wa Rias, Wabunge na Madiwani, Sura ya 343 kikisomwa pamoja na kanuni ya 13(4) ya Kanuni za Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani za Mwaka 2025 imetoa kibali cha waangalizi wa uchaguzi kwa taasisi na asasi za ndani ya nchi nne (04) kwa uchaguzi mdogo tajwa.

Tume inatumia nafasi hii kuzipongeza taasisi na asasi za kiraia zilizopata kibali cha kutoa elimu ya mpiga kura na kuwa waangalizi wa wakati wa Uchaguzi Mdogo wa Ubunge katika Jimbo la Peramiho na Udiwani katika Kata ya Shiwinga.

Imetolewa na:

Kailima, R. K.

**MKURUGENZI WA UCHAGUZI**